TUONYESHE BABA ITATUTOSHA

. . . na mimi, tulikuwa tumeketi hapa tukizungumza sisi kwa sisi, Mimi na Ndugu Thomas, na Ndugu Rhodes, ambao tulikuwa ndio kwanza tupate majaliwa ya kukutana, nasi tulikuwa, bila shaka, tukiwa na ninii, mnajua jinsi tulivyo na ucheshi kidogo, wahudumu wanao, mwajua, kwa namna fulani tulikuwa, kile nilichotaka kuzungumzia asubuhi ya leo nilipokuwa hapa, lakini si—sina wakati, cha *Kutoa Presha Kidogo,* basi hiyo ndiyo njia pekee tuliyo nayo ya kutoa presha, ni wakati tunapokuwa na u—ucheshi kidogo.

2 Na ndugu mzee mtauwa, mtakatifu, ambaye ndiyo kwanza aende Utukufuni, ambaye karibu sisi sote tunamfahamu, alikuwa Ndugu F. F. Bosworth, naye daima alikuwa na ucheshi mwingi. Nilikuwa nikisitasita kidogo kuhusu kuangalia na kusikiliza, kwa sababu ninataka "Ndiyo, ndiyo," na "La, la." Nilipomwona mzee huyu mcha Mungu na ucheshi aliokuwa nao, kisha nikawaona watumishi wengine mashuhuri, Ndugu Vayle, na hawa ndugu wengine hapa na hao wote, walipokutana pamoja, walikuwa na ucheshi kidogo, basi nikawazia, "Vema, labda hiyo ndiyo de—desturi tu ya siku hizi za mwisho, miongoni mwa wahudumu."

3 Halafu nilikuwa nikisoma katika *Baraza Lililotangulia Nikea*, na *Waanzilishi Wa Nikea*, na kadhalika, baadhi ya hao watumishi mashuhuri wa Kristo katika miaka iliyopita, nao walikuwa na ucheshi, nanyi mwajua, hatimaye nikaja kuona kwamba Mungu ana ucheshi, kwa hiyo . . .

4 Basi tukizungumza juu ya ushirika, nilikuwa nikiwazia mmoja ambapo Ndugu Bosworth alikuwa akisema, aliniambia, akasema, "Ndugu Branham, unajua *ushirika* ni nini?"

Nikasema, "Naam, ninaamini najua."

5 Akasema, "Ni 'jamaa wawili katika meli moja.'" Kwa hiyo hilo ndilo . . . Mnaweza kuwa karibu sana pamoja pale, mwajua; kwa hiyo huo ni *ushirika*. Na bila shaka huu ni wakati mzuri sana, wa ushirika.

6 Sasa, nilikuwa . . . Wakati mimi, unapokuwa mzee kidogo, si—siwazii upesi kama nilivyofanya nilipokuwa kijana, kama Ndugu Parker hapa. Mimi . . . Yeye, akizungumza muda mfupi uliopita, alisema sikuzote anamwambia mkewe ya kwamba yeye mke anazeeka naye anakuwa kijana, na kadhalika. Nami ninajaribu hiyo nyumbani pia, lakini haifanyi kazi vizuri sana. Vema, kama unaweza kuifanya ifanye kazi au la, lakini—lakini, hata hivyo, nilipomwambia tu, kuna tofauti ya miaka kumi tu katika umri wetu, nikasema, "Wewe fuatilia barabarani miaka kumi zaidi, na badala ya kuisukumia mbali Biblia hiyo namna

hiyo, itakubidi kuiangalia kwa miwani, basi, unapokuwa mzee kidogo."

7 Na kwa hiyo, tumefurahishwa sana na mkutano huu na matokeo yake. Nami nilikuwa na wakati kidogo, Ndugu Parker hapa alikuwa akinielezea baadhi ya Ma—Maandiko, nami najua yale ninyi nyote mnayopitia huko chini je—jengoni, huko chini maskanini, juu ya mafundisho haya ya Maandiko. Na jinsi, ni njia nyenyekevu, tamu jinsi gani aliyoiendea, kuniambia kuhusu mambo fulani, ambayo nilimwambia mara alipoyaandika kwenye karatasi fulani, akaniachia, nipate kuketi chini, niyasome. Nami ninapenda njia hiyo (Nanyi je?), kwa mtu fulani, ambaye hajaribu kushindilia kitu fulani ndani yako, bali kuliacha tu kwa unyenyekevu na utamu.

8 Hivi majuzi . . . siku kadhaa zilizopita nilikuwa nikizungumza na ku—kundi la ndugu, ambao walikuwa, wa dhehebu fulani, kwa kweli walikuwa wakinivuta kwenye makaa, nao wakasema, "Ni upuuzi kuhubiri uponyaji wa Kiungu." Loo, jamani! Walijua Kitabu chote, mwajua, na kusema, "Mbona, siku hizo zimepita, muda mrefu uliopita!"

Nikasema, "Vema, mahali fulani, Ndugu, umerudi tena, kwa sababu mimi—mimi—mimi hakika ni . . . "

9 Nao walikuwa wakiniambia basi, kwamba sikupaswa kujaribu kuhubiri bila kuwa na elimu, bila kwenda kwenye shule ya Biblia na kujifunza jambo fulani, nami ni—nikangojea tu mpaka walipomaliza, ndipo nikasema, "Mnajua," nikasema, "nawaambia, ninyi ndugu kweli hamna budi kuwa na wakati mzuri sana," nikasema, "mwajua, katika makosa na hatia zangu zote, na Yeye—Yeye ananipenda jinsi anavyonipenda, na ni vigumu kwangu kuvumilia jambo hilo wakati mwingine." Nikasema, "Nashangaa juu ya hao walio katika ile kweli, sijui jinsi yeye, wao wanavyoweza kulivumilia basi," mwajua, loo, kulipenda namna hiyo. Nikasema, "Ni kunena- . . . "

10 Katika—katika kosa hili lote tunalodhaniwa kuwa nalo, mwajua, na kama anatupenda hivi, vipi kuhusu wale kweli walio na ile kweli? Ninawazia kweli wana wakati mzuri, sivyo? Kwa hiyo tutabaki tu jinsi tulivyo mpaka atakapotuonyesha kosa letu, ndipo, tutasonga mbele tuingie kwenye kile wanachodhani ni kweli, kama Yeye akisema ni kweli, nalo Neno Lake linalitangaza.

11 Na kwa hiyo, lakini katika kundi kama hili ndipo mahali pa karibu sana na Mbinguni palipo duniani. Wakati sisi hapa tumeketi pamoja asubuhi ya leo, tayari tumekufa, kazi hiyo imekwisha, nasi tume—tumezikwa, hiyo ni kweli, sote tumezikwa, na halafu tumeninii, isitoshe, bali tumefufuka tena. Tumefufuliwa na katika Kristo katika kufufuka Kwake, sisi ni sehemu yake. Na sasa tunakusanyika pamoja katika ulimwegu wa Roho *katika* Kristo Yesu. Mnaona? Tuko ndani Yake kwa

ubatizo, mnaona, "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja," na sisi hapa, sasa tumekusanyika, Mwili wa Bwana Yesu.

12 Na sasa, ibada zenu zinaanza katika yapata dakika thelathini, ama, dakika thelathini na tano, basi kama ningejaribu kutumia somo hili la *Kutoa Presha*, tungekuwa tukiitoa hadi adhuhuri, nami nadhani labda, tutakuwa tukiitoa vizuri. Lakini nilifikiri labda ningechukua tu ushuhuda mdogo wa jambo fulani, ndipo—ndipo basi tunaweza kurudi kanisani.

13 Ningependa kuwa humo na kuketi chini ya mafundisho ya hawa watumishi mashuhuri wa Kristo, Ndugu Vayle, Ndugu *pale* juu, na Ndugu yetu mpendwa Parker, na Ndugu Iverson, na wengi wa ndugu wengine hapa, na ningependa kuwasikiliza. Alikuwa akiniambia utaratibu wa huo mkutano, "kumwacha Roho atende kazi," napenda hilo, halafu mtu mwingine anayeinuka anaendeleza hayo katika upatanifu. Sasa, huyo ni Roho Mtakatifu, hiyo ni kweli. Lakini unapoona kwamba mtu mwingine anaingia na ukanushaji, basi hiyo ni, hiyo inavunja wakati huo wa ushirika, inavunja ninii. . .mnaona, kuna kasoro katika hilo.

14 Sasa, nilimwambia Ndugu Parker, wakati akinialika kwa fadhili wakati mmoja, labda—labda mwaka ujao kama Bwana akikawia, huenda nikarudi nami ningetaka kushuka na—na kuwa na siku nzima kuketi tu pamoja na hao ndugu na kuzungumza juu ya ujuzi wangu binafsi, wa jinsi, kukutana na Roho Mwenyewe.

15 Huwezi kuzungumza mbele ya ulimwengu huko nje, mambo hayo. Kama ukisema jambo fulani, nimeliangalia, nena tu neno, na mmoja atalichukua na kuegemea upande *huu* nalo, na huyo mwingine alichukue na kuegemea upande *ule* nalo, na muda si muda mwajua, haliambatani na mada kuliko yale wewe. . .na halafu linaingia miongoni mwa watu, na wengine wakasema, "Ndugu Branham anasema *hivi*." Na hilo, vema, si kwangu tu, ni kwa ndugu yeyote namna hiyo. Kwa hiyo kuketi tu pamoja na wahudumu, ambapo mna majaliwa ya kuinuka, na hilo ndilo linalowafanya safi, ni wakati unapoweza kuketi chini na kusikiliza, na kugawa mawazo ye—yenu pamoja.

16 Sasa, ninathamini wakati huu wote mzuri sana. Ninaomba maombi yenu ninapoingia, sina budi kwenda, sasa, chini kusini kutoka hapa hadi Columbia, kisha nifanye hima kurudi nyumbani. Ninafika nyumbani Jumatano usiku, ninaondoka Alhamisi asubuhi. Ninafika nyumbani Jumatano usiku, saa tatu, saa nne, ninaondoka yapata saa kumi Alhamisi alfajiri kwenda kwenye Pwani ya Magharibi kuanza ibada kwenye Ikulu ya Ng'ombe. Na kutoka hapo. . .Hiyo ni yale makubwa ya mifugo, Maonyesho ya Mifugo ya Magharibi huko Lango la Kusini, California. Kisha tuondoke huko na kuendelea hadi

Grass Valley, na huko ni karibu, juu kuelekea Nevada, na kisha kuedelea kwenye, hadi kwenye jimbo la Maonyesho ya Ulimwengu mwaka huu, na kisha kuingia Canada. Nasi kwa namna fulani tumepangiwa ratiba, tukingojea kuwaona, ninyi, kwenda California kutoka . . . kuingia Alaska kutoka huko. Kwa hiyo niombeeni.

17 Nami ninamthamini Ndugu Parker na upendo wake mkuu, na, kwa kunialika kuja hapa kwenye mkutano wake mkuu, na majaliwa ya kuniachilia huru jukwaani niseme lolote Mungu angeweka moyoni mwangu kusema, ninamthamini mtu mtauwa. Na, Ndugu, Dada, niliwazia asubuhi ya leo, kuzungumza tu nanyi kutoka moyoni mwangu.

18 Hamna milango mingi mno iliyofunguliwa kwangu. Nami, bila kushikilia jambo hili dhidi ya ndugu zangu, hata kidogo, bali ninaamini wakati mwingine kwamba, ni kama tu nilivyosema, watu wanachukua msimamo mbaya na kuegemea upande *huu* na upande *ule* nalo, nalo linasababisha mchafuko miongoni mwa ndugu, nami ninaweza kuona wao ni wachungaji, nami ninaweza kuelewa hilo, bila shaka nimekuwa nikilitarajia, nami niliamini ya kwamba lingetokea.

19 Nami nina imani yangu mwenyewe, kama kila mhudumu alivyo nayo. Sijaribu, miongoni mwa makusanyiko, kujaribu kupanda mafarakano, kwa sababu hilo ni jambo moja analochukia Mungu, ni mafarakano miongoni mwa ndugu, lakini ninapokuwa huko nje mikutanoni, na—najaribu kushikilia makuu, ningeyaita, nadhani, mafundisho makuu ya kimsingi, ya kiinjilisti na Mafundisho ya Biblia, yale ya kimsingi: kuonekana binafsi kwa Yesu, na kifo cha kimwili, kuzikwa, kufufuka, kupaa juu, na kurudi, na kadhalika, ninafundisha tu mambo hayo, uponyaji wa Kiungu na kadhalika, ambayo, sisi sote watu wa full Gospel hakika tunakubaliana juu ya hayo.

20 Nami nawatakeni, ndugu, mjue ya kwamba kanda ninazofundisha kanisani mwangu mwenyewe ziliingia miongoni mwenu, na kadhalika, ama, miongoni mwa makusanyiko yenu, nami nina imani yangu mwenyewe. Na—na, bila shaka, sasa, kuachilia imani yangu, nisingefanya hivyo, kwa sababu ningekuwa mnafiki, mnaona, ni—ningekuwa mnafiki kufanya hivyo. Kwa hiyo na—naamini yale niliyofundisha kwenye kanda, ninaamini kila Neno Lake. Nisingewalisha watu kitu kibaya. Na iwapo nimekosea, basi na—naomba ya kwamba Mungu atanisamehe hilo, kwa sababu Hivyo ndivyo vizuri sana ninavyofahamu.

21 Na kwa hiyo, lakini kunialika hapa na kuwa na hawa wahudumu, kundi zuri la wahudumu wanaoketi hapa asubuhi ya leo, watu watauwa . . . Nami nilikuwa kwenye . . . Ndugu mwenye fadhili si muda mrefu uliopita, na dada, samahani, nilikuwa huko Phoenix, na mkutano mzuri sana pamoja na ndugu

wa thamani, ninayempenda, naye aliniita chumbani mwake, alikuwa mwaminifu sana, naye akasema, "Ndugu Branham," akasema, "unajua ninakupenda."

Nami nikasema, "Asante, ndugu yangu, hakika ninakupenda."

Naye akasema, "Unajua, tunaona kana kwamba huduma yako kwa namna fulani imekuwa nzuri sana."

22 Nikasema, "Loo, usiseme hivyo." Nikasema, "Ni... Sininii...Hilo si sawa." Nikasema, "Nilimfuata tu Bwana, nawe umefanya vivyo hivyo, kwa hiyo sisi sote..." Nikasema, "Angalia jinsi alivyokubariki, zaidi ya vile alivyowahi kunifanyia, na mambo makuu ambayo amekupa." Nikasema, "Kamwe hakunifanyia mambo hayo." Kisha nikasema, "Inalazimu kuchukua pesa nyingi sana, wa—wala kamwe sikuchukua pesa, kwa sababu nadhani angeninii, wajua, Yeye, labda asingeweza kuniamini nikiwa nazo." Mnaona? Nami nikasema, "Mimi...Jambo lingine," nikasema, "huduma yangu ndogo, nisingeweza kwenda mahali padogo sana kama..."

23 Hivi majuzi tu nilifanya mkutano ambapo, ulikuwa na watu ishirini tu, lakini Bwana aliniongoza kule. Nami ni—ninataka kwenda mahali anaponiongoza, sihitaji pesa, mnaona, nami na—nataka tu kwenda popote ninapojisikia kuongozwa kwenda.

24 Na hivi majuzi, hata katikati ya shida hizi zote, niliangalia kwenye vitabu vyetu, na ni miji mia tatu, au zaidi, miji mikubwa Marekani inayoniita nije kwao, kwa hiyo, mbali na nchi za kigeni. Basi nilikuwa...Ndugu huyu akasema, "Vema, haya ndiyo ninayotaka kukwambia, Ndugu Branham," akasema, "wewe—wewe una—wewe una msimamo mkali sana."

25 Nikasema, "Vema, mimi ni Muairishi kwa—kwa kuzaliwa, kuzaliwa kwa kwanza, Myahudi kwa pili." Kisha nikasema, "na sisi," nikasema, "basi, unajua, hayo, hebu changanya hayo pamoja," nikasema, "ni vigumu kusema ungekuwa na nini." Nami nikasema, "Labda," nikasema, "Mimi—mimi kwa kweli ni mkali, nadhani ni asili yangu tu kuwa hivyo, ninaenda tu kwa moyo wote. Ninapowazia chochote ni sawa, ninauza tu kila kitu nilicho nacho, unaona." Tena nikasema, "Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Kristo, kwangu mimi.

26 "Na sasa, watu wangu walionitangulia, huko nyuma, walikuwa Wakatoliki," nami nikasema, "kutoka Ayalandi, wote wanatoka Dublin." Ndipo nikasema, "Ndipo wao, ambao... Nilisikia habari za ninii, nilipokuwa mvulana mdogo, mambo yaliyotukia, na kulikuwa na wito maishani mwangu.

27 "Halafu Wakatoliki wakasema, 'Sisi ndio Kanisa,' na kuwafungia hao wengine nje; ninaenda kwa Mlutheri, wanasema, 'Sisi ndio Kanisa,' na kuwafungia wengine wote nje." Nikasema, "Yapata mia sita, mia saba, ama labda madhehebu mia tisa mbalimbali, tutajuaje lililo sahihi? Kwa

hiyo nikaichukua tu Biblia, ninadumu tu na jinsi ninavyoisoma, na kuiweka tu namna hiyo."

Naye akasema, "Vema, hili hapa jambo moja," kasema, "daima unawakemea hao wanawake." Hmm? Akasema . . .

Nikasema, "Ninawaonea tu wivu."

28 Akasema, "Unawaambia jinsi wanavyopaswa kuvaa, na yote kuhusu ati wao ni wazinifu kupindukia, na—na ati hawapaswi kuvaa nguo hizo, na hizo kaptura, na ati waache kukata nywele zao na mambo haya mengine yote uliyosema." Kasema, "Unashambulia hayo." Akasema . . .

"Vema," nikasema, "hayo yako katika Maandiko."

Kwa hiyo akasema, akasema, "Vema, ninajua hilo pia."

Nikasema, "Hivi huamini hilo, ukiwa mhudumu wa Kipentekoste?"

Akasema, "Naam, lakini," kasema, "Ndugu Branham," akasema, "watu wanakuamini wewe kuwa ni nabii."

Nikasema, "La, sivyo."

29 Akasema, "Lakini wanakuamini hivyo," akasema, "nawe unapaswa kuwa ukiwafundisha wanawake hao jinsi ya kupokea karama kuu za kiroho na mambo kama hayo," tena kasema, "basi—basi Ka—Kanisa lingekuwa bora zaidi."

Nikasema, "Ndugu . . . "

Akasema, "Ikiwa umeenda kilindi zaidi na Mungu, wafundishe watu kwa kilindi zaidi na Mungu."

30 Nikasema, "Ninawezaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawatasikiliza ABC zao namna hiyo?" Mnaona? Mnaona? Nikasema, "Vipi? Wakati," nikasema, "sisi . . . ? . . . Basi hiyo ni karibu tu . . . "

31 Akasema, "Vema, Ndugu Branham, naweza kukufanyia jambo fulani?" Akasema, "Ninaamini kama ungeachana tu na hilo, na uendelee tu na kuwaombea wagonjwa . . . " Nami . . . "Na—na kuliachilia. Mungu alikuita, waombee wagonjwa."

Nikasema, "Hiyo ni kweli."

Akasema, "Basi, liache tu liende hapo." Unaona? "Achana tu nalo uende ukawaombee wagonjwa."

Nikasema, "Lakini vipi kuhusu hili lingine?"

Akasema, "Wala na mimi siamini hilo. Lakini," kasema, "unajua nini? Kama ningesema kitu kama hicho, mbona," kasema, "wangefanya *hivi*, *vile*."

32 Nikasema, "Haya basi." Mnaona? Mnaona? "Haya basi," Mnaona? Nikasema, "Tusipolitetea, basi ni nani atakayelitetea?" Mnaona? "Kizazi hiki hakina budi kuhukumiwa." Ndipo nikasema, "Basi halina budi kutoka mahali fulani."

Akasema, "Vema, nitakwambia nitakalofanya, utaniruhusu nikuwekee mikono na kuomba ya kwamba Mungu atayafungua macho yako uione kweli?"

Nikasema, "Nitakubali chini ya sharti moja, kama utaniruhusu nikufanyie vile vile."

33 Kasema, "Vizuri sana." Kwa hiyo tukaombeana. Natumaini itanisaidia sana, na hakika ninatumaini. Natumaini kwamba, natumaini maombi yake yatanisaidia, kwa sababu mimi... kama...ni—ni—ni—ninataka kusaidiwa, nipo hapa kwa kusudi hilo.

34 Sasa, ni dakika ishirini na tano tu sasa mpaka ibada yenu itakapoanza, lakini hebu nisome tu neno moja kutoka katika Biblia hapa, na kuzungumza tu, ama, kutoa ushuhuda, kisha tutaondoka. Mathayo 5:8, ama, hebu tuone, ninaamini nitasoma zaidi ya hayo. Nina jambo lingine ninalotaka kusoma, ndio kwanza linijie akilini, kama ninaweza kulipata sasa, mahali tu lilipokuwa. Kama...Ninaamini ninaweza, sina hakika sana nalo. Sina budi ku—kusoma jambo fulani hapa kutoka kwa Yohana Mtakatifu. Naam, ninataka kulisoma kutoka hapa, Yohana Mtakatifu, mlango wa 6, hebu tuanzie yapata—yapata mlango wa 6 na kifungu cha 36:

> *Lakini naliwaambia, Kwamba* ninyi *nanyi mmeniona wala hamwamini.*
>
> *Wote anipao Baba watakuja kwangu; wala ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe.*
>
> *Kwa kuwa mimi sikushuka kutoka mbinguni ili niyafanye mapenzi yangu, bali mapenzi yake aliyenipeleka.*
>
> *Na mapenzi yake Baba aliyenipeleka ni haya, ya kwamba katika wote* alio...*alionipa nisimpoteze hata mmoja, bali nimfufue siku ya mwisho.*
>
> *Na mapenzi yake aliyenipeleka ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele: nami nitamfufua siku ya mwisho.*
>
> Yesu...(Samahani.) *Basi wale Wayahudi wakamnung'unikia, kwa sabahu alisema, Mimi ni chakula kilichoshuka kutoka mbinguni.*
>
> *Wakasema, Huyu siye Yesu, Mwana wa Yusufu, ambaye twamjua babaye na mamaye? Sasa asemaje huyu, Nimeshuka kutoka mbinguni?*
>
> *Basi Yesu akajibu, akawaambia, Msinung'unike ninyi kwa ninyi.*
>
> *Hakuna mtu awezaye kuja kwangu,* asipovutwa *na Baba* Yangu *aliyenipeleka: nami nitamfufua siku ya mwisho.*

Imeandikwa katika manabii, Na wote watakuwa wamefundishwa na Mungu. Basi kila mtu aliyesikia na kujifunza kutoka kwa Baba, huja kwangu.

Si kwamba mtu amemwona Baba, ila yeye atokaye kwa Mungu, huyo ndiye aliyemwona Baba.

. . . amin, naambia . . . Amin, amin, nawaambia, Yeye aniaminiye mimi yuna *uzima wa milele.*

Mimi ndimi chakula cha uzima.

35 Nilikuwa tu nikiwazia, nilipokuwa nimeketi hapa mezani, na muktadha wangu mdogo wa somo nililokuwa nimeandika huko nje, *Kutoa Mvuke*. Niliwazia asubuhi ya leo, "Ni kitu gani kinachowafanya watu kuendesha . . . ?" Ni—nina rafiki hapa ambaye ametoka huko mbali Texas, na—na kote nchini, nina marafiki walioketi hapa kutoka Canada. Nasi tuna marafiki kutoka kila mahali katika kundi hili dogo la watu asubuhi ya leo, baadhi yetu ni wahudumu, wengine ni wafanya kazi, wake wa nyumbani, na kadhalika, na kusudi letu la kukusanyika pamoja ni nini?

36 Wengi wenu nyote huja kila mwaka kumsikiliza ndugu yetu wa thamani na mafundisho yake, na wengi wenu husoma makala yake, nami nimeyasoma, nami nafikiri ni ya maana sana. Daima, Billy, ambaye ndiye katibu wetu wa uamsho, hunihifadhia lile *Kilio Cha Usiku Wa Manane* kila wakati, kwa sababu ninapenda kusoma ya Ndugu Parker, njia yake ya kuyaendea Maandiko, nanyi mnayasoma, nanyi mna—mnayawazia. Ndipo wakati mikutano inapokuwa, tunakusanyika pamoja, ni kwa sababu kuna kitu fulani ndani yetu kinachotamani ku—kusikia zaidi, ku—ku—kushika kitu fulani, ni Uzima. Hakuna neno kuu zaidi tunaloweza kuwazia asubuhi ya leo kuliko *Uzima*. "Asiyemwamini Mwana hataona Uzima."

37 Jinsi mtu hana budi kuwa kipofu ambaye hawezi kuona Uzima! Na kuwazia ya kwamba watu wengi hawaoni Uzima. Sasa, huenda tukauona, bali neno *kuona* halimaanishi kuangalia, neno *kuona* linamaanisha "kuuelewa." Sasa, Yesu alimwambia Nikodemo, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi *kuuona* Ufalme." Sasa, kwa maneno mengine, utakuwa ukiangalia kitu fulani nawe useme, "Sikioni," unamaanisha *hukielewi*. *Kuona*, kile tunachoita "kuona," huko ni "kuangalia." Lakini *kuona* katika istilahi za Biblia ni "kuelewa kile tunachoangalia, kufunuliwa." Nasi tunakusanyika pamoja namna hii kusudi Kristo apate kufunuliwa miongoni mwetu, hiyo ndiyo sababu ya mikutano mikubwa kufanywa. Na kitu kikuu kama Uzima . . .

38 Nilikuwa nikiwazia juu ya ushuhuda ambao huenda nikautoa wakati huu, kuchukua tu dakika zingine kumi, kumi na tano. Nilihubiri wakati mmoja, labda hapa, nimehubiri mahali kadhaa, juu ya *Tuonyeshe Baba Itatutosha*, na *Kumwona*

Mungu Ametuzunguka Kote. Mzee mmoja alikuwa anaishi huko chini mtoni, ametuacha sasa, naye alikuwa mvuvi mzee, mvulana wake mdogo alikuwa akipanda mtoni na kuvua samaki pamoja naye. Maskini jamaa huyo, siku moja akishuka mtoni, alikuwa. . . Mvua ilikuwa imekuja na kuziosha anga kutokana na mavumbi na majani yote kutoka kwenye miti, ndipo upinde wa mvua ukatokea u—upande wa magharibi, ama, mashariki, nao walikuwa wakielekea magharibi kwenye Mto Ohio.

39 Ndipo yule mzee mvuvi akaanza, machozi makubwa yakitiririka mashavuni mwake alipokuwa akiutazama huo upinde wa mvua. Ndipo jamaa huyo mdogo akashikwa na shauku sana, akasimama chomboni, katikati ya hiyo mashua, akasema, "Bwana, nataka kukuuliza swali." Kasema, "Mchungaji wangu hawezi kulijibu, mama yangu, mwalimu wangu wa shule ya Jumapili," kasema, "ikiwa Mungu ni mkuu sana," kasema, "mbona mtu asiweze kumwona?"

40 Ndipo hu—huyo jamaa mzee, akiwa amelemewa na matamshi ya huyo jamaa mdogo, akamkumbatia, akasema, "Nakutakia heri, kipenzi, yote niliyoona kwa miaka hamsini imekuwa ni Mungu," Mnaona? Angeweza kumwona Mungu, kuona Uzima. Mungu ni Uzima, Uzima ni Mungu.

41 Michache, yapata miaka miwili iliyopita, rafiki yangu mwema, akiketi hapa ndani mahali fulani, na mimi, tulikuwa huko chini Kentucky tukiwinda kuchakulo, tukitoa mvuke kutoka mkutanoni. Nasi tulikuwa tumepiga kambi nje, nami nilikuwa mchafu, na hii ni fidhuli sana kutoa tamshi kama hili mbele ya ndugu, sikuwa nimeoga kwa majuma mawili, na kwa hiyo—kwa hiyo ni—nilikuwa kabisa, kabisa, vema, nilihitaji sana kuoga. Kwa hiyo—kwa hiyo, lakini mimi na Ndugu Wood, yeye alikuhitaji sana kadiri nilivyokuhitaji, kwa hiyo hatukuangaliana wakati sisi. . . kwa hiyo sisi. . .

42 Kulikuwa kukavu sana huko mwituni, na ndevu zetu zimetokeza usoni mwetu, na kwa hiyo tukaenda. . . Kuchakulo, wao, ukikanyaga kichakani, mbona, wanaweza kukusikia, na, loo, jamani, Houdini, bingwa wa kutoroka, hana chochote kwa mmoja wa hao jamaa wadogo. Na huko chini wanapopita, wanarushiwa risasi kwa vyovyote vile, wanakuwa wakali, wanatoroka tu. Naye akasema, "Mimi. . . "

43 Nikasema, "Ndugu Wood, laiti tungaliweza kupata mahali palipokuwa na vibonde. . . " Sijui kama hawa. . . Ndugu, unajua. . . ? Ni wangapi wanaojua kibonde ni nini? Jamani, hilo ni sawa. Ni, mwajua, handaki inayopitia msituni, na kwa kawaida hapo maji hutiririka na kutiririka chini, nayo huyalowesha majani.

44 Nikasema, "Kama tungekuwa na ninii. . . " Huu ulikuwa ni msitu mkubwa, tambarare tuliokuwa tukiwindia, nami nikasema, "Laiti tungeweza kupata mahali palipokuwa na

vibonde vikubwa vyenye kina kirefu ambamo chemchemi huyadumisha," nikasema, "tungeweza kuwapata kuchakulo vizuri zaidi."

Naye akasema, "Loo, ninajua mahali kama hapo."

Nikasema, "Vema, tutaenda."

45 Nasi tukaingia kwenye gari na kuondoka kwenye kambi yetu, na tulipokuwa njiani kule, akasema, "Ndugu Branham," akasema, "Nataka kukwambia," kasema, "afadhali uniache nizungumze."

Nikasema, "Vema, hakika umekaribishwa."

Naye akasema, "Mtu huyu ni kafiri, na, loo, yeye ndiye mbaya kuliko wote nchini."

Nikasema, "Ve—vema, wewe zungumza basi."

Kwa hiyo—kwa hiyo akasema, "Nafikiri huenda ananijua." Bw. Wood alitoka huko chini katika nchi hiyo.

46 Kwa hiyo tukaenda mpaka mahali pale, nasi tukaendesha gari huko nyuma kupitia mashambani, na kushuka kupitia kwenye uwazi, na kupanda juu ya vilima. Na kwa hiyo, sikuwa nimewahi kuwa humo nchini. Na kwa hiyo, tulipofika pale mahali *fulani* hapa, mbona, tulisimama kwenye nyumba kubwa kule nyuma, na kulikuwako na wazee wawili wameketi huko nje, wenye umri mkubwa sana, nadhani katika miaka yao ya sabini, wameketi chini ya mtofaa, kivulini, tukaendesha pale, Bw. Wood akatoka, nami nikasikia msemo wa kale wa Kentucky, "Ingia."

47 Unajua, hivyo ndivyo wanavyowaita Waindiana, "Mahoosia." Mnaona? Jinsi walivyopata hilo, katika siku za mwanzoni, huko Kentucky, hiyo ilikuwa ni huko kusini, kwa hiyo unapokuja kwenye nyumba ya kusini, huko chini kusini, wangesema, "Halo," ungesema, "Ingia." Haidhuru ulikuwa ni nani, mradi tu ulikuwa unatembea, ulikuwa umevaa viatu, ama kama hukuvaa viatu, ingia kwa vyovyote vile, umekaribishwa.

48 Lakini ulipovuka mpaka ukaingia Indiana, kidogo walishuku, ukisema, "Halo," walisema, "Ni nani hapo?" Wanataka kujua kwanza. Nina furaha mimi ni mkusini, na kwa namna fulani ninalipenda hivyo.

Na kwa hiyo a—akasema, "Ingia."

Kwa hiyo Bw. Wood akapanda juu, akasema, akamwita mtu huyo kwa jina, akasema, "Wewe ndiye?"

Kasema, "Mimi ndiye yule msumbufu."

49 Kwa hiyo akasema…Nikaona alikuwa jamaa mkali sana, nami nikasema…nimeketi kwenye gari. Ndipo Bw. Wood akasema, "Ningetaka kukuomba…" Akasema, "Kwanza nataka kujitambulisha," akasema, "jina langu ni Wood, Banks Wood." Naye akasema, "Mimi, ninawinda kuchakulo, nami nimekuwa hapa mahali *fulani*, na," akasema, "ni misitu

tambarare, na kumekauka sana kule, tulijua unamiliki ekari kadhaa hapa zilizokuwa na vibonde, ndipo nikawazia, labda ningekuja huku na kukuomba, nawe ungeniruhusu kuwinda."

Yule mzee akatema kitafuno chake kikubwa cha tumbaku na akasema—akasema, "Wewe ni mvulana wa Jim Wood?"

Akasema, "Naam."

Akasema, "Jim Wood . . . "

50 Sasa, walikuwa ni Mashahidi wa Yehova, mwajua. David, yeye (nakisia walifika humu asubuhi ya leo; wanauza vitabu pale mkutanoni.), mguu wake ulikuwa umekunjamana chini yake, na—na Bw. Wood, akiwa ni Shahidi wa Yehova, alikuwa amehudhuria mmoja wa hiyo mikutano, na kabla sijaondoka kwenye jengo hilo Roho Mtakatifu alikuwa ameniambia kungekuwako na mvulana pale, na kusema, "Jina la baba yake litakuwa ni 'Wood,' nao wanatoka Kentucky ya kusini." Kisha kasema, "Ana polio." Kisha kasema, "Sema neno, atatembea." Ndipo nikaangalia pande zote kuona lile ono, nisingeweza kumwona mvulana huyo, nami nikaendelea, baada ya kitambo kidogo nikamwona huko nyuma kabisa, nikaita jina lake, hapo mguu wake ukanyoka, mnaona, kwa hiyo hakuwa Shahidi wa Yehova tena.

51 Nimeninii, kwa neema ya Mungu, nimeongoza kila mmoja wa familia yake, baba yake msomaji wa Mashahidi wa Yehova, wote kwa Kristo na ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kuwabatiza wote tena, kwa hiyo basi—kwa hiyo basi, kwa maono, yale Bwana angetoa, na kusema mambo ambayo yangetukia.

52 Kwa hiyo basi, akasema, "Mtu yeyote—mtu yeyote aliye na uhusia- . . . " Kasema, "Mvulana wa Jim Wood anaweza kuwinda popote anapotaka." Kasema, "Karibu tu." Kasema, "Nina ekari mia tano hapa za msitu usioguswa, fanya tu utakacho."

Akasema, "Nimeambatana na mchungaji wangu, hutajali kama akienda?"

Akasema, "Wood, usiniambie umeshuka chini vya kutosha hata inakubidi kubebana na mhubiri popote uendapo."

Na kwa hiyo akasema, "Vema . . . " Kasema . . .

53 Nami niliwazia wakati umewadia, mimi kutoka basi, mwajua, kwa hiyo nikatoka kwenye gari na kuzunguka kando, kisha nikasema, "Mu hali gani?" Naye Bw. Wood alikuwa anaenda kunitambulisha, kabla hajapata wakati wa kufanya hivyo . . . Na, loo, masharubu ya majuma mawili, na damu ya kuchakulo, inanuka kama kicheche. Kwa hiyo ni—ni—nikaanza kuzunguka pale, nami nikasema, "U hali gani, Bwana?"

Akasema, "Nawe ni mhubiri ati?"

Nikasema, "Vema, ningependa kuwa." Nikasema, "Mimi . . . "

Naye akasema, "Vema, ninaninii tu . . . Unajua," akasema, "Ninachukuliwa kuwa ni kafiri."

Nikasema, "Si jambo kuu la kujivunia, sivyo, Bwana?"

Naye akasema—akasema, "La, nadhani sivyo." Akasema, "Kuna jambo moja tu nililo nalo dhidi yenu ninyi jamaa."

54 Nami nikasema, "Naam, Bwana, kama ni jambo moja tu basi, uko na hali nzuri sana." Baadhi ya wale ambao nimekutana nao, walikuwa . . . Nina Wakristo wengi, ambao, wanadhaniwa kuwa, wana zaidi ya hilo dhidi yangu. Kwa hiyo, nikasema—nikasema, "Vema, hilo—hilo ni zuri sana."

Akasema, "Kile nilicho nacho dhidi yenu enyi jamaa ni hiki: Daima mnapiga makelele juu ya Kitu ambacho hamjui chochote kukihusu."

Nikasema, "Kwa mfano, kitu gani, Bwana?"

Naye akasema, "Mnazungumza juu ya Mungu, wala hakuna Kitu kama hicho."

"Loo." Nami nikasema, "Hicho ndicho?"

Akasema, "Naam, hamna lingine."

Nikawaza, "Bwana, Wewe nisaidie."

55 Sasa, kuna njia mbili tu za kukiendea chochote, ndugu zangu, hizo ni njia sahihi na njia mbaya. Nafikiri, hebu nisimame hapa kidogo katika hadithi yangu, na kusema nafikiri hiyo ndiyo shida yangu na wengi wetu ndugu, tuna bidhaa *nzuri sana* hapa, lakini tunauendea umma vibaya kupita kiasi, na kutufanya watu wa kujitenga. Mnaona? Itajiuza, iishi tu, mnaona. "Ninyi ni chumvi ya dunia." Na chumvi, mradi tu ladha iko katika chumvi hiyo, itaokoa kama ikigusa. Lakini kama imepoteza ladha yake, haidhuru tunapaza sauti jinsi gani hapa chini, na tunaruka juu na chini jinsi gani, inabidi kuwe na Maisha hapa nje unaounga hilo mkono.

56 Kwa hiyo nikamwangalia yule mzee muungwana, nikawazia, "Bwana, maskini jamaa huyu mzee, ameuchimba maskini udongo huu hapa. Baba yangu angaliishi, angalikuwa kwenye umri huo, yapata umri huo. Sasa, kuna kitu fulani kidogo tu hapa ambacho Wewe ungeweza kunisaidia kusema, hapana shaka, kipate kumsaidia mzee huyo kuona." Nami nimeona wengi wanaojiita makafiri, nami nimesimama karibu na baadhi yao walipokuwa wakituaga, wao si makafiri, wanaondoka tu, mnaona. Na kwa hiyo . . . Huo ni msemo wa mitaani, lakini hivyo ndivyo mtakavyouelewa, unaona, "kuondoka," na, kutoa mvuke.

Nami nikasema, "Vema, ni . . . Hayo ni, bila shaka," nikasema, "hayo ni maoni, bila shaka."

57 Ndipo tukasimama pale kwa dakika moja, nasi tulikuwa tumeketi chini ya mtofaa. Akasema, "Nimekuwa kwenye mikutano hiyo, nao ni kama tu mbwa mdanganyifu." Akasema,

"Nilikuwa na maskini mbwa mdanganyifu, nami nikampiga risasi." Akasema, "Ningemfuata kila usiku, nimpeleke hapa nje naye angekuwa akibweka, na kupanda kule juu, naye anapaswa kuwa mbwa wa kuuni," kisha kasema, "kuuni angekuwa juu ya mti," akasema, "basi muda si muda mwajua, angekuwa akibwekea juu ya mti huu namna *hiyo*, nami ningezunguka pale na kuuangazia wote juu, huyo kuuni alikuwa tayari ametorokea huko juu."

Nikasema, "Lakini, Bwana, hata hivyo, huyo kuuni alikuwako, yeye ni mbwa tu." Unaona? Natumaini alipata kile nilichomaanisha, nami nina hakika mmekipata.

58 Kwa hiyo akasema, "Kwa hiyo nikampiga risasi." Naye akasema, "Si—sipendi chochote kitakachodanganya. Nami nafikiri kama mtu akiongea, anapaswa kuwa anajua anachozungumzia."

Nikasema, "Bila shaka nakubaliana nawe."

59 Akasema, "Kulikuwa na mhubiri mmoja niliyemsikia, ambaye kama nikimwona mtu huyo," kasema, "Sijawahi kumsikia, bali nilisikia habari zake, kama nikipata kumwona mtu huyo, nitamsikiliza."

Nami nikasema, "Hilo ni zuri sana."

Akasema, "Alikuja mahali padogo hapa panapoitwa Acton, kwenye uwanja wa kambi wa Methodisti." Ndipo Ndugu Wood akaniangalia, nami nikatikisa kichwa changu.

60 Akasema, "Maskini Dada *Fulani-wa-fulani* huko juu kilimani hapa," ninasahau ninii lake. . .kamwe hakumwita "Dada," "Bi. *Fulani* ana umri wa kama miaka sitini na mitano," kasema, "alikuwa yuafa kwa kansa tumboni." Kisha kasema, "Alikuwa na madaktari kutoka Louisville hapa, na," kasema, "wana shamba zuri huko juu," halafu kasema, "wangeweza kuyagharimia. Wakampeleka Louisville kwa ajili ya upasuaji, haukufaa kitu hata kidogo, wakampasua, wakamshona, kansa ilikuwa tayari imemshika kote."

61 Kasema, "Alikuwa akifa taratibu hapa kwa miezi kadhaa." Kasema, "Hatimaye alifikia mahali ambapo alikuwa mahututi sana, nami. . . " Samahani Ndugu yangu, Dada. Kasema wao. . . Nitalielezea tu jinsi alivyolisema. Hata asingeweza kufika kwenye maliwato ya kitandani wasingeweza kamwe kuweka moja chini yake, wasingeweza kumwinua juu hivyo, iliwabidi kutumia shuka la kuvuta, shuka la mpira, na kisha shuka la kuvuta.

62 Kasema, "Mimi na mke wangu tulienda kule kila asubuhi na tungebadilisha, mke wangu angebadilisha kitanda chake, nami ningesaidia kutoa hilo shuka chini yake, na kadhalika." Kisha kasema, "Yeye alikuwa tu. . .Daktari alisema wampe tu mofini kidogo ama chochote kile, wapate kumstarehesha iwezekanavyo

mpaka atakapokufa." Kasema "Alikuwa na yapata majuma mawili ya kuishi."

63 Basi akasema, "Kuna mhubiri aliyekuja hapa chini kutoka Indiana, naye alikuwa na . . . huku kwenye uwanja wa kambi wa Kimethodisti." Akasema, "Kulikuwa na mamia kadhaa ya watu waliokusanyika kule, walisema, kumsikiliza mhubiri huyu." Naye akasema, "Ndipo usiku huo," kasema, "alipokuwa akihubiri," kasema, "dada yake alikuwa ameketi kule nyuma, ambaye alikuwa ni Bibi *Fulani-wa-fulani* anayeishi hapa kwenye kilima kingine." Kisha kasema, "Mhubiri huyu alidhaniwa kuwa na *kitu fulani*, hata angeweza kuwaambia watu kuhusu yale waliyokuwa wamefanya, na kwa nini walikuwa wagonjwa, na yote kuhusu hayo." Kisha kasema, "Nilikuwa nimesikia habari zake, lakini bila shaka, sikuamini jambo la kupindukia kama hilo."

64 Naye akasema, "Lakini hata hivyo, mwanamke huyu usiku huo alikuwa ameketi mkutanoni. Basi wakati mhudumu alipokuwa akizungumza, alimgeukia mwanamke huyu, naye ameketi nyuma ya jengo, na kusema, 'Ulipoondoka nyumbani, usiku wa leo, huko nyuma, Bibi *Nanii*,' kasema, 'ulichukua maskini les- . . . ama, leso ndogo yenye mchoro wa bluu pembeni mwake kutoka kwenye kabati, ukaitia kwenye pochi yako.' Kisha kasema, 'Unamwombea huko nyuma dada yako mkubwa ambaye yuafa, jina lake ni *Fulani-wa-fulani*, anayeishi hapa juu kilimani.' Kasema, 'Bwana ameyasikia maombi yako. Sasa, chukua leso hii ndogo uiweke juu ya dada yako, nayo kansa hiyo itamwacha.'

65 "Vema," kasema, "karibu yapata usiku wa manane usiku huo, nilifikiri walikuwa na Jeshi la Wokovu kando ya kilima kule juu, mayowe yote na kupiga makelele."

66 Sitaki kumwaibisha mtu yeyote, lakini huyo alikuwa ni Ben, aliyeketi hapa, Ndugu Ben. Mnajua mlio huo unaojulikana wa "Amina," anaoutoa kila usiku mkutanoni kule chini, ambao hupatikisa mahali hapo. Ndugu Ben alikuwa amempeleka huyo mwanamke kule juu, yeye, kwa dada yake, naye alikuwa amemwekea leso hiyo, ndipo Ben akaamini. Kwa hiyo akaanza tu kupaza sauti kabla halijatukia, kwa hiyo alikuwa tu akiliendea kwanza. Kwa hiyo Ndugu Ben . . .

67 Akasema, "Nilifikiri huyo mwanamke alikuwa amekufa. Vema," kasema, "ilikuwa yapata usiku wa manane, kwa hiyo kesho yake asubuhi," kasema, "mimi na mke wangu tukaenda kule." Kisha kasema, "Unajua nini?" Kasema, "Mwanamke huyo alikuwa ameamka, akipika kiamshakinywa chake, akila sambusa za matofaa zilizokaangwa."

68 Ni wangapi wenu ninyi waasi mnaojua sambusa ya tofaa iliyokaangwa ni nini? Loo, jamani, nazipenda mno! Ninapenda waipake sukari ya rojorojo. Mnaona? Na mimi—mimi—mimi

si Mmethodisti, mimi ni Mbaptisti, ninapenda kuzibatiza kwa sukari ya rojorojo, mwajua, kuipaka kwa wingi, kisha uzile, siagi moto na, mmmm!

69 "Kwa hiyo basi wakati alipokuwa akila hizi sambusa za matofaa," na kusema "karibu iniangushe mimi na mke wangu." Kisha kasema, "Na kama huamini hilo," akaelekeza kidole chake, kasema, "Nitakupeleka moja kwa moja kule juu na kukuonyesha huyo sasa hivi. Yeye ni . . . "

Naye yule mzee aliyeketi pale, akasema, "Hiyo ni kweli." Huyo mzee mwingine, mnaona.

Nami nikasema, "Loo, ninakuamini."

70 Akasema, "Wananiambia mtu huyo anakuja hapa Campbellsville, kwenye uwanja wa michezo." Kisha kasema, "Ninaenda kule kumsikiliza, nami nitazungumza naye."

Kasema, "Naam, Bwana."

71 Naye akasema, "Nami nitamwuliza ni kitu gani hicho ambacho kingeweza kumwambia habari za mwanamke huyo, na kujua ya kwamba atapata afya." Kasema, "Sasa, sielewi kabisa."

72 "Loo," nikasema, "hilo ni la ajabu kweli," nikasema, "bila shaka ni la ajabu." Nami nikawaza, "Bwana, nisaidie sasa, sijui niseme nini tena." Lakini ninakumbuka maskini mama yangu alivyozoea kuniambia, "Mpe ng'ombe kamba ya kutosha, atajinyonga," mwajua. Kwa hiyo hilo—hilo ni karibu tamshi zuri la kusini ambalo ni kweli. Nikawaza, "Nitaona tu jinsi anavyojali kweli, nitamwondosha kwenye hiyo hoja." Nikasema, "Utajali kama nikiokota moja ya hayo matofaa?"

Akasema, "Manyigu wanayala, naam unaweza kuchukua moja."

73 Mnajua nyigu ni nini? Wakifyonza tu matofaa, na ilikuwa yapata katikati ya Agosti. Niliokota moja na kulipangusa kwenye maskini suruali chafu iliyojaa damu, na kuliuma, nikasema, "Jamani, ni tamu sana!"

Kasema, "Loo, naam, linapendeza."

Nikasema, "Je, ni—ni muda gani . . . Mti huo una umri gani?"

"Loo," naye akasema, "Nilipanda kitu hicho."

Nikasema, "Loo?"

74 Akasema, "Kina umri wa miaka arobaini na minane hivi." Akasema, "Unaona mahali lile dohani la kale limesimama kule juu kilimani?" Kasema, "Nilizaliwa kule juu." Akasema, "Na—na wakati babangu alipokufa," akasema, "tulikuwa tumejenga nyumba hii hapa chini," kisha kasema, "ndipo nikahamia hapa chini, na watoto wangu wote wamezaliwa huku chini." Kisha kasema, "Ni—nimeishi hapa tangu wakati huo. Nami niliupanda huo mti hapo, kitu kidogo sana, basi ni—nimekua tu pamoja na huo mti."

Nikasema, “Naam, Bwana, kumbe.” Nikasema, “Ninaona hayo matofaa yote yanaanguka.”

Akasema, “Naam, naam.”

Nikasema, “Majani yanapukutika.”

“Naam, Bwana.”

Nikasema, “Ajabu hiyo, sivyo?”

Akasema, “Una maana gani?”

75 Nikasema, “Unajua, hatujakuwa na jalidi, na hata hivyo majani hayo yanaanguka.” Ndipo nikasema, “Hiyo ndiyo sababu tumekuja hapa kuwinda humu kibondeni, majani mitini yanapukutika.” Nami nikasema, “Nashangaa ni kwa nini yanapukutika kabla hayajapata jalidi yoyote?”

“Loo,” akasema, “yana—yanapukutika kabla hayajakuwa na jalidi.”

Nami nikasema, “Naam, Bwana.” Nami nikasema, “Ni kitu gani kinachoyafanya yapukutike?”

Akasema, “Vema, u—uhai uliyaacha.”

Nikasema, “Kumbe. Basi huo uhai ulienda wapi?”

Akasema, “Ulishuka chini ya huo mti, ukaingia kwenye shina la mti.”

“Loo, kumbe.” Nikasema, “La sivyo, kama jani hilo lilibaki pale juu, nao uhai ukabaki kule juu, ungeshikilia hilo jani pale.”

“Loo, naam.”

Nami nikasema, “Halafu jani linatoka mtini, linarudi chini kwenye shina kujificha.”

“Naam.”

Nikasema, “Kwa nini unashuka kuingia huko chini?”

76 “Vema,” akasema, “kama ungekaa huku juu, majira ya baridi kali yangeuua m—mti huo. Huo uhai hauna budi kushuka chini kwenye shina, katika ardhi yenye joto, kuhifadhi uhai, upate kuleta jani lingine msimu ujao wa kupukutika.”

“Loo,” nikasema, “Kumbe. Na kila wakati unapopanda juu unakuletea lundo la matofaa na kadhalika?”

“Naam, hiyo ni kweli.”

Nikasema, “Vema, Bwana, ningetaka kukuuliza swali.”

Akasema, “Vema.”

77 Nikasema, “Naomba uniambie, ni Akili gani inayoliambia jani hilo kabla ya hapo, ama, uhai huo huko juu kwenye mti huo, ni Akili gani inayouambia uhai huo—huo, ‘Toka huku juu ukaingie mizizini, kwa sababu usipofanya hivyo utakufa’”? Kisha nikasema, “Halafu—halafu kwenye majira ya vuli mwakani, unachipusha jani lingine.” Nikasema, “Sasa, ni kitu gani kinachoufanya ushuke chini kwenye shina la huo mti?”

"Loo," akasema, "ni maumbile kwa maji kushuka."

78 Nikasema, "Vema. Labda nitaweka ndoo ya maji kwenye nguzo hapa nje, ndipo mnamo katikati ya Agosti yatashuka chini ya hiyo nguzo, kisha yarudi tena majira yajayo ya kuchipua?"

"La, hayatafanya hivyo."

Ni—nikasema, "Kwa nini yasifanye hivyo?"

"Vema," anasema, "si maumbile kwake."

79 Nikasema, "Kwani maumbile ni nini? Ni nani anayeyatawala maumbile? Ni kwa nini basi hayafanyi hivyo kwa msonobari? Yanakaa hapa juu. Ni tofauti gani inayoyafanya . . . inayotofautisha tofauti kati yao?"

80 Yule mzee akatafakari kidogo. Nikasema, "Unaona, Bwana," nikasema, "inabidi kuwepo na Akili fulani, kwa sababu mti huo hauna akili, hauna budi kuongozwa. Si kifaa cha kimitambo, ni Akili inayoutuma huo uhai chini kwenye shina la mti, kama vile kifo, kuzikwa, na kufufuka." Aliishi miaka hiyo yote wala asingeweza kuona uhai.

81 Nikasema, "Nina . . . " Mimi ni mmishenari, nami nimesikia yote, ninakwambia hili, nimesikia mawazo yao yote mbalimbali, Buddha, Baniani, na—na nadharia mbalimbali, lakini zote ni za uongo. Ukristo umewekewa msingi juu ya kuzikwa na kufufuka, sio kuzaliwa tena, ufufuo. Sio, kuleta kitu kama hicho, kitu kile kile kilichoshuka, kinapanda juu, Yesu yeye yule.

82 Kama utaangalia, Mungu huyashuhudia maisha yetu kila siku: Asubuhi jua huzaliwa, saa nne liko kwenye utineja wake, adhuhuri liko katika nguvu zake zote, kisha linatua jioni (Je, huo ndio mwisho wake?), halafu linachomoza tena. Kuzaliwa, kuishi, kufa, kufufuka, daima, Mungu akishuhudia maishani. Mti hurudi chini, utomvu unaingia mashinani upate kuleta uhai tena mwaka ujao. Sisi, wewe na mimi, tunaning'inia kwenye Mti wa Uzima, sisi ni—sisi ni tunda la Mti huo.

Yule mzee, baada ya kuketi pale kidogo, alisema, "Sikuwazia hilo kamwe."

83 Nikasema, "Hujajibu swali langu, ninataka uniambie ni Akili gani inayotawala uhai huo katika mti huo unaoshuka chini. Hiyo, Akili hii inaweza kuzungumza na uhai huo, sio huo mti, ule uhai," Uhai ulio ndani yako, unaona, "inaudhibiti uhai huo, na kuurudisha hapa chini na kuuficha," (kama vile Ayubu alivyosema, "Ficha . . . Ungenificha kuburini, uniweke mahali pa siri"), "na kisha inaurudisha tena katika majira ya kuchipusha." Wala asingeweza kunijibu.

84 Nikasema, "Akili ile ile inayozungumzia uhai katika mti huo na kusema, 'Jifiche iwapo unatarajia kuishi,' hiyo ndiyo Akili ile ile iliyoniambia la kumwambia mwanamke huyo, jinsi ya kuishi, kuamini."

Akasema, "Wewe siye yule mhubiri?"

Nikasema, "Naam, Bwana, ndimi."

85 Hapo uwanjani siku hiyo, kwa hadithi ndogo rahisi, ninajua kumechelewa, nimeninii sana. . . ninapaswa kuwa nimeondoka, nina. . . kuna mengine zaidi yanayoambatana nayo, lakini kwenye uwanja huo siku hiyo, kwa kitu kidogo rahisi tu cha huyo mtu kuona tu uhai, nilimwongoza kwa Kristo.

86 Mwaka jana nilirudi tena na mjane wake alikuwa ameketi barazani nilipokuja, akakutana nami. Huku mikono yake ikiwa imeshikana na yangu, akasema, "Ndugu Branham, alikufa katika imani ya Bwana Yesu. Ametuacha."

87 "Yeye amwaminiye Mwana atakuwa na. . . anaweza kuona Uzima." Si vigumu kwetu basi, kwamba tunaweza kuona kwamba kuna Kitu fulani kinachoyatawala maisha yetu. Hayo ndiyo tunayotafuta, Uzima, na huo kwa wingi zaidi. Nami ninamwomba Mungu, asubuhi ya leo, katika kiamshakinywa hiki kwamba tutakuwa na Uzima mwingi. Na Yeye, anayeweza kusema na huo mti kwa akili Zake, nao huo mti upesi unatii wito wa Bwana wa kujificha, kama unatarajia uhai. . . Nami ninajua mahali pengine pazuri pa kujificha ili kuhifadhi Uhai, hebu tujifiche hapo asubuhi ya leo, si katika kinga ya bomu, bali chini ya mbawa Zake, hebu tujifiche. Twaweza kuomba?

88 Baba yetu wa Mbinguni, loo, tunajua ya kwamba leo, hata sasa, tumefunikwa tu na uhai, tunauhisi, tunaona jua likichomoza, kutua. Tunaangalia maua yanapochanua, halafu jalidi inayapiga, na msafara wa mazishi unakuja, mvua ya msimu wa majani kupukutika inanyesha, na kububujisha machozi makubwa na kuyazika, yanalala kaburini na kuoza, lakini huo sio mwisho wake, Wewe umeyahifadhi maisha yao. Ndipo mara tu jua, j-u-a, linapoanza kuchomoza, haidhuru kama mbegu hiyo, imewekelewa jiwe kubwa, au yadi za zege zimemwagwa juu yake msimu wa baridi kali, ambapo mbegu hiyo imezikwa, wakati jua hilo lenye joto linalotawala uhai wa mimea linapoanza kuipasha dunia joto, mbegu hiyo inachipuka.

89 Tunaona nyasi zetu nyingi sana ziko moja kwa moja kando ya hiyo njia. Ni ile mbegu iliyozikwa chini pale, haiwezi kuficha uhai. Uhai hauna budi kuchipuka. Tunaweza kuuweka kwenye kikapu, na halafu, tuuzike chini ya kikapu, tukitundike kikapu hicho mtini, bali maskini uhai huo utakua kwa sifa za Mungu.

90 Ee, Mungu, jalia tusiwe na akili ndogo sana, finyu sana, bali tuangalie tu pande zote na kumwona Mungu kila mahali. Na ni zaidi sana jinsi gani tunavyoweza kumwona asubuhi ya leo, katika watoto Wake wapendwa, tunaposhiriki pamoja hapa *katika* Kristo Yesu, Ambaye ni Uzima!

91 Jalia kila msafiri, Bwana, sisi si wa ulimwengu huu, sisi ni wasafiri na wageni, sisi ni wasafiri, na kama wasafiri kutoka Georgia, kutoka Canada, kutoka Texas, kutoka kila mahali

huku, tumekutana pamoja hapa katika sehemu hizi ndogo kubadilishana mawazo yetu, na kutoa shuhuda zetu za utukufu Wake, jalia tuondoke kwenye mkutano huu tukiwa na wingi wa Uzima wa Milele tupate kuwafundisha wengine njia ya kuupata. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Asanteni.

92 [Ndugu fulani anasema, "Hebu tuendelee kuketi na kumwacha Ndugu Branham aondoke, kama angetaka, kama ungependa kuondoka Ndugu Branham."—Mh.] Loo, hilo ni sawa. ["Najua inawabidi kuendelea. Ndipo tutaendelea na ibada zetu, kwa hiyo tutangojea mpaka atakapoondoka hapa."] Asante. ["Hatutaki kukuondoa, lakini nafikiri hili ni bora zaidi." Sehemu tupu kwenye kanda.]

93 . . . nami nimechukuliwa kama mtu anayejitenga, lakini sivyo nilivyo, mnaona. Na—napenda ushirika, lakini hapa, ni—ninafanya mkutano kule chini, nitashuka mara moja. Nyote mna Uzima wa Milele, kwa hiyo aminini tu. Lakini hapa, mahali padogo tu kisha nianze kuzungumza na watu, mnaona, kama kuna jambo lolote baya, likianza kukusumbua, wewe lishike, unaona, na unapofanya hivyo, basi, unaona, linanirarua tu vipande-vipande kwa ajili ya jioni tena, mnaona. Nami nina hakika Wakristo wanaelewa hilo, mnaona.

94 Ni-. . . si kwamba siwapendi. Jamani, ni . . . kama isingalikuwa ni kwa ajili yenu, vema, huduma yangu ingekuwaje? Vipi kuhusu wale walio huko nje? Haidhuru huduma ingekuwa kubwa jinsi gani, haiwezi kuwa kubwa mpaka mwifanye kubwa. Siwezi kufanya hivyo mimi mwenyewe, inahitaji mimi na ninyi pamoja kuifanya, mnaona. Peke yangu, si kitu, peke yako, si kitu, bali sisi pamoja, Bwana huleta huduma Yake. Kama hamngeiamini, isingetukia kamwe, inawapasa kuiamini, basi hilo ndilo linaloifanya itendeke, kwa sababu mnaiamini. Mungu awabariki.

62-0609B Tuonyeshe Baba Itatutosha
Jefferson Inn
Southern Pines, North Carolina Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org